

Namna ya kuzuia maambukizo ya kifua kikuu sugu:

- Mshauri mgonjwa afunike mdomo na pua kwa kitambaa safi pindi anapokohoa au kupiga chafya
- Mwelekeze mgonjwa ateme makohozi/ mate kwenye kopo lenye mchanga na amwage kwenye shimo na kufukia
- Hakikisha madirisha ya chumba cha mgonjwa yanakuwa wazi ili kuruhusu mwanga na hewa safi ya kutosha
- Mshauri mgonjwa aepuke misongamano isiyokuwa ya lazima



Kwa maelezo zaidi wasiliana na mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

kupitia
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma
S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.
Barua pepe: info@moh.go.tz,
Tovuti: www.ntlp.go.tz,
Toleo la 2016



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Majukumu ya Msimamizi wa matibabu ya mgonjwa wa kifua kikuu (TB) sugu katika ngazi ya jamii



TB SUGU INATIBIKA NA KUPONA

Utangulizi

- Mgonjwa wa kifua kikuu sugu huanzishiwa matibabu katika kituo cha kutolea huduma za kifua kikuu sugu, baadaye huendelea na matibabu nyumbani chini ya usimamizi wa mtu yeyote aliyechaguliwa na mgonjwa mwenyewe
- Msimamizi huyu hutekeleza majukumu yafuatayo ili kufanikisha tiba sahihi kwa mgonjwa

Umezaji wa dawa

- Msindikize mgonjwa kila anapohudhuria kwenye kituo cha tiba kuchukua dawa
- Hakikisha mgonjwa anaonwa na daktari kwa uchunguzi kila mwezi na inapohitajika
- Fahamu aina za dawa, dozi na muda wa kumeza
- Fuata ratiba ya matibabu ya mgonjwa
- Msimamie na hakikisha mgonjwa anameza dawa inavyotakiwa
- Tambua na toa taarifa ikiwa mgonjwa atapata maudhi au madhara yanayotokana na dawa

Vipimo wakati wa matibabu

- Hakikisha vipimo vya ufuatiliaji wa matibabu vinafanyika kwa wakati:

| Aina ya kipimo | Lini kifanyike |
|---------------------|--|
| Kipimo cha makohozi | Kila mwezi |
| Kipimo cha damu | Kila mwezi |
| Uzito | Kila mwezi |
| X-ray | Kila inapohitajika na baada ya kumaliza matibabu |

Elimu na ushauri

- Toa elimu ya kifua kikuu sugu kwa familia ya mgonjwa na jamii
- Mshauri mtu mwenye dalili za kifua kikuu anayeishi na mgonjwa kwenda kwenye kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi
- Shirikisha familia na jamii namna ya kumsaidia mgonjwa kupata lishe bora
- Msisitize mgonjwa kuhusu ufuasi sahihi wa dawa za kifua kikuu sugu

Maudhi ya dawa za kifua kikuu sugu na hatua za kuchukua

| Maudhi | Hatua ya kuchukua |
|-------------------|--|
| Kichefuchefu | Mgonjwa aendelee na dawa na toa taarifa kwenye kituo cha tiba |
| Kutapika | Mgonjwa aendelee na dawa na toa taarifa kwenye kituo cha tiba |
| Maumivu ya viungo | Mgonjwa aendelee na dawa na anaweza kunywa dawa za kupunguza maumivu kama paracetamol, pia toa taarifa kwenye kituo cha tiba |

Madhara ya dawa za kifua kikuu sugu na hatua za kuchukua

| Madhara | Hatua ya kuchukua |
|----------------------|---------------------------------------|
| Kuwashwa mwili mzima | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Kutokwa vipele | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Kizunguzungu | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Kutosikia vizuri | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Uoni hafifu | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |

Madhara ya dawa za kifua kikuu sugu na hatua za kuchukua

| Madhara | Hatua ya kuchukua |
|-------------------------------------|---------------------------------------|
| Msongo wa mawazo na kuchanganyikiwa | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Macho au ngozi kuwa rangi ya njano | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |
| Kupoteza fahamu | Mpeleke mgonjwa kwenye kituo cha tiba |

Lishe kwa mgonjwa wa kifua kikuu sugu

- Shauri familia ya mgonjwa kuhakikisha kwamba mgonjwa wa kifua kikuu sugu anapata lishe bora ambayo ni chakula chenye mchanganyiko wa makundi yaliyo orodheshwa (aina moja kutoka kila kundi):
- Vyakula vya kujenga mwili; mf. dagaa, maharage, nyama nk.
- Vyakula vya kuupa mwili nguvu; mf ugali, wali, viazi nk.
- Vyakula vya kulinda mwili; mf. matembele, mchicha, kisamvu, matunda nk.
- Vyakula vya kuupa mwili joto; mf. siagi, karanga, korosho nk.

Kumbuka:

- Mgonjwa ale angalau milo mitatu kwa siku (asubuhi, mchana na jioni)
- Mgonjwa anywe maji safi na salama ya kutosha